

Wilaya ya Columbia School Namba 93
Fomu ya Ruhusa na Idhini - Safari za Kielimu

Kama sehemu ya mpango wa elimu wa Columbia Public School, wilaya hutoa fursa za elimu za nje ya shule ("safari za kielimu"). Wakati mwingine wanafunzi hupelekwa hadi katika shule nyingine za CPS au majengo ya shule kwa hali hizi za kielimu, ikiwa ni pamoja na lakini si tu kwa CPS Nature School au kwa shule ya kati au shule ya upili ambako mwanafunzi atajiunga, au kwenye ukumbi kwa tamasha. Wakati mwingine wanafunzi hupelekwa maeneo yasiyo ya shule, ikiwa ni pamoja na lakini si tu kwenye bustani ya wanyama, jumba la makumbusho, au uwanja wa muziki. Wilaya itawasiliana na wazazi kwa barua pepe, jarida, nakala za karatasi zinazotumwa nyumbani na wanafunzi, au ujumbe, taarifa kuhusu ya safari hiyo na tarehe na saa za safari hizi. **Kama hutaki mwanafunzi wako ashiriki, tafadhali mjulishe mwalimu au mkuu wa shule kwa maandishi kabla ya tarehe ya safari ya kielimu.** Kwa kutia saina fomu hii, unakubali yafuatayo:

- Ninaidhinisha mwanafunzi aliyetajwa katika hati hii kuhudhuria safari za kielimu za wilaya, isipokuwa nimjulishe mwalimu au mwalimu mkuu wa mwanafunzi wangu kwa maandishi kabla ya tarehe ya safari ya kielimu. Ninatambua kuwa uvunaji wa kanuni zozote unaweza kusababisha mwanafunzi kurudishwa shuleni mara moja, kwa gharama yangu. Ni jukumu langu kukutana na mwanafunzi kwenye uwanja wa ndege, kituo cha basi, n.k., kama itahitajika ili kumpeleka mwanafunzi nyumbani kutoka katika safari ya kielimu ya nje ya mji.
- Ninaidhinisha wafanyakazi, wakandarasi, watu wa kujitolea au wafanyakazi wengine wa matibabu wa CPS, wakiona kuwa inahitajika kwa busara na hiari yao, kupata au kutoa huduma ya matibabu kwa mwanafunzi wangu, kumpeleka mwanafunzi wangu katika kituo cha matibabu na kupata matibabu (ikiwa ni pamoja na lakini si tu huduma ya afya ya kawaida au ya dharura, kulazwa hospitalini, kudungwa sindano, kudungwa dawa ya kutia ganzi au upasuaji) yanayozingatiwa kuwa yanahitajika kwa afya ya mwanafunzi wangu. Ninakubali kulipa gharama zote zinazohusiana na matibabu na usafiri huo na ninakubali kutolewa (kwa au na CPS) rekodi yoyote ya matibabu inayohitajika kwa makusudi ya matibabu, kupewa rufaa, kutoza bili au bima.
- Mimi na mwanafunzi wangu tunawajibika kwa hatari yoyote inayoweza kutokea kutokana na usafiri wa mwanafunzi wangu kwenda, kushiriki na kurudi kutoka katika safari iliyoelezwa hapo juu. Ninakubali kuwajibika kikamilifu kwa gharama yoyote na zote za matibabu ya majeraha au ugonjwa wowote unaotokea kwa mwanafunzi wangu kutokana na usafiri wa mwanafunzi wangu kwenda, kushiriki na kurudi kutoka katika safari iliyoelezwa hapo juu.
- Ninathibitisha kwamba nimesoma hati hii kwa makini na ninakubaliana na masharti yake kwa ufahamu na kwa hiari. Ninathibitisha pia kuwa mimi ni mzazi au mlezi halali wa mwanafunzi aliyetajwa katika Fomu hii. Ninaelewa kuwa nina uwezo wa kukataa kutia saina fomu hii. Kama sitatia saina fomu hii, mwanafunzi wangu hataweza kushiriki katika safari ya kielimu isipokuwa wilaya ipate idhini tofauti kutoka kwangu kwa kila safari.

Kwa hivyo, ninampa mwanafunzi wangu, _____, (jina) _____, (namba ya mwanafunzi/namba ya chakula cha mchana) ruhusa ya kushiriki katika safari za kielimu. Nitamjulishe mwalimu wa mwanafunzi wangu kwa maandishi kabla ya tarehe ya safari ya kielimu ikiwa mwanafunzi wangu hawezi kushiriki. Kama mwalimu hajajulishwa, mwanafunzi wangu ana ruhusa ya kuhudhuria safari ya kielimu.

(JINA LA MZAZI/MLEZI)

(SAINI YA MZAZI/MLEZI)

(TAREHE)

Bima ya matibabu **inependekezwa lakini haihitajiki**. Taarifa zifuatazo, zikitolewa kwa wilaya, zitatolewa katika hali ya dharura inapohitajika ili kupata usaidizi wa matibabu kwa mwanafunzi wako.

Jina la Kampuni ya Bima ya Matibabu

Simu (_____) _____ Namba ya Bima _____

Daktari wa Mwanafunzi _____ Simu (_____) _____ ----